**Kanuni ya Madhara**

Mara nyingi nashangaa kwa nini wapagani wanaichukia dhana isemayo “wapagani hawana viwango vya malengo” ili kuchunga maisha yao. Walakini wapo wapagani wengi ambao hawana tatizo kukubali kuwa hawana na viwango halisi vya malengo linapokuja suala la maadili, lakini wengine hawaonekani kulikubali.

Tofauti na Wapagani, Wakristo wana viwango vya malengo na wanaishi kwa viwango hivyo. Wanatambua kuwa Yesu ana mamlaka mbinguni na duniani, Mathayo 28:18-20 na kwamba kila tufanyalo lazima lifanywe kwa mujibu wa mamlaka yake, Wakolosai 3:17. Wakristo wanafanya hivyo kwa sababu Mungu amewakirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, 2 Petro 1:3. Ongeza, wakristo wanatambua kuwa maneno ya Yesu ndiyo yatakayowahukumu wanadamu tutakaposimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, Yohana 12:48-50; 2 Wakorintho 5:10.

Hivyo, Mungu hutufundisha cha kufanya, tusichotakiwa kufanya ili tumpendeze. Mfano mkubwa wa hili ni ule unaopatikana katika Wagalatia 5. Hapa, Mungu anamtajia mwanadamu matendo ya mwili, “ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, Ibaada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yafananayo na hayo”. Mungu anaendelea kutofautisha hayo matendo ya dhambi na tunda la Roho ambalo ni “upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria. Neno la Mungu limejaa maelezo kama yaliyopo katika Wagalatia 5, ambapo kiwango cha malengo huwekwa, huwasilishwa na kukubaliwa na wale wamwitao Bwana. Hata kwa kusema hivyo, bado, si wote wanaodai kuwa Kristo ni Bwana wanaishi kama ambavyo Kristo angetaka waishi. Kwa maana wale wanaodai jambo moja na kuishi vingine, Biblia inatufundisha kuwa Mungu atawahukumu, Waebrania 6:4-6; Mathayo 7:21-23; 2 Wathesalonike 1:7-9. Maana Mungu si Mungu wa machafuko, 1 Wakorintho 14:33.

Sina tatizo na kukubali kuwa kuna viwango vya malengo. Kama ambavyo sina tatizo na kukubali kuwa kuna watu wanaodai kuwa wanaishi kwa viwango, wakati wanavikana, wanavifedhuri, na kuvikanganya kwa sababu zao binafsi. Nina

uelewa finyu vya kutosha kusema kuwa wale wanaokikataa, kukifedhuri na kukikanganya kiwango cha malengo hawataokoka, Mathayo 7:21-23. Ni Yesu aliyesema kuwa njia iendayo mbinguni ni nyembamba, Mathayo 7:14. Hivyo, swali si tu ungamo la mdomo bali utiifu, Waebrania 5:9.

Ndiposa swali linabaki,ki wapi kiwango cha malengo kwa ajili ya upagani? Mpagani yeyote asikudanganye kwa sababu hawana kiwango adilifu cha malengo. Mwongozo wao ni wanachodhani kuwa ni " jema bora." Kama wanalazimika kuongopa,kupunja, kubaka, kuua n,k. kwa ajili ya kufikia "bora mradi jema",wamefungwa na kiwango chao kutenda hayo.

Natambua kuwa wapagani wengine wanachukizwa na hili na wengine wangependa "kunirukia kooni" kwa sababu ya maelezo niliyotoka kuyatoa. Walakini, kimsingi wapagani wanatakiwa kukubaliana kwenye jamii yao wenyewe kabla hawajanijibu na kutegemea niwasikilize. Najua "wapagani hawana kiongozi mkuu." Pengine, bwana Richard Dawkins, mpagani maarufu wa siku hizi, ametembea ng'ambo na ng'ambo ya bahari kuwasimika watu kadha wa kadha kuwa wasemaji wa upagani wa kimarekani. Mmoja wa watu hao ni bwana Dan Baker, rais mwenza wa *Freedom From Religion Foundation,* asasi kubwa ya kipagani Marekani. Baker na watu walio kama yeye wako wazi katika kile wanakichukulia kuwa kiwango chao cha maadili au ukosefu wa kiwango cha maadili. Nakili zifuatazo kutoka kwa Baker na wengine zitaonyesha kwamba hata viongozi wa upagani wanakubali kuwa hawana kiwango cha malengo. Sasa, endapo wapagani wenzao wana daawa juu ya nakala hizi, msinisumbue mimi, wasumbueni wao…..wekeni nyumba yenu katika utaratibu, kabla hamjathubutu kuirarua ya kwangu. Kuhusiana na kiwango anachotumia, Baker alisema "kanuni ya madhara kama kiwango chake." [1] Aliendelea kusema "thamani halisi hutoka katika ubinadamu, hali ya miiko katika ulimwengu halisi," [2] Hili liko sawa na Charless Darwin aliposema, "Tazama, endapo una mtu ambaye haamini katika Mungu basi unachoweza kujitahidi kufanya ni kile anachojisikia kuwa ni bora kwake, hicho ndicho anachohitaji kufanya." Ni kama utiifu, eti?

Katika mdaharo na Peter Payne, Baker alitanabaisha, "Vitendo vyote hutegemea mazingira. Hakuna kitendo ambacho ni chema au kibaya." Kwa maelezo hayo,

wakati wa madaharo na Kyle Butt, Baker aliulizwa “ endapo ubakaji ungekubalika katika hali fulani.” Katika hoja hiyo, Baker alitanabaisha, “ingetisha, ingejutisha. Nigejichukia, na pengine ningejiua baada ya kubaka. Ningekuwa na ujasiri Endapo hiyo ndiyo ingekuwa namna pekee-namna pekee, ningefanya. Ningemwonea huruma huyo mwanamke, nigejionea huruma mimi mwenyewe. Lakini maadili yangenitaka kuchukua hatua ya kivitendo ambacho kingesababisha madhara madogo.” Kwa hiyo Baker yuko wazi kwamba, mpagani mwaminifu angekuwa na ujasiri wa kutenda jambo fulani la kusikitisha kama ubakaji endapo tendo hilo lingepelekea ambacho anakitetea kuwa “kiasi kidogo cha madhara.” Sifahamu ni wahanga wangapi wa uababakaji wangekubaliana na fikra hii. “ubakaji huo ni mwanana katika mazingira fulani” Sasa unaweza kujibu kuwa hakusema ni mwanana, sawa, alisema, maadili yangenitaka.”

[1]http://www.youtube.com/watch? V=8otGP_kINBI

Mwana-midhaharo msomi “mkubwa” anatambua ambacho upagani unayafanyia maadili. Humfanyia  mungu wake mwenyewe; hakimu wake mwenyewe, kiapo chake mwenyewe; Hakimu wake ni kile kinachoonekana kuwa madhara madogo katika kila hali. Zingatia alichosema Baker, “Kama nataka kuwa mwadilifu, nitachukua hatua ya kivitendo itakayosababisha kiasi kidogo cha madhara.”[1]

Jamani, ni rahisi. Huyu kiongozi wa upagani hataki kuambiwa cha kufanya. Badala yake wanataka kuumba mungu-mtu wa kwao. Au twaweza kusema kuwa iko hivi; wanataka kuchukua nafasi ya Mungu.  Zingatia asemacho Nietzsche “Mungu ni mwambato; lakini nataka mwambato wenu usipitilize utashi wenu wa ubunifu. Unaweza kumuumba Mungu? Basi, usiniambie kuhusu miungu iwayo yote. Lakini unaweza kumuumba mungu-mtu.” Na hiki ndicho walichikofanya! Wapagani wajifanya “miungu-watu” juu ya Mungu.

“Basi, nitakutenda hivi, Ee Israeli, na kwa sababu nitakutenda hivi, ujiweke tayari kuonana na Mungu wako, Ee Israeli” Amosi 4:12